

NJIA YA MUNGU

ILIYOANDALIWA

KWA AJILI YETU



Pamoja sasa, ishikilieni, kubwa sana sasa.

Neema ya ajabu! jinsi inavyosikika ni tamu,
Iliyomwoko mwovu kama mimi!
Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, lakini sasa
nimepatikana,
Nilikuwa kipofu, bali sasa ninaona.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru kwa ajili ya majaliwa makuu tuliyo nayo ya kuja Kwako. Kwanza, hatuwezi kuja isipokuwa kwa njia ya Kristo. Kwa hiyo basi tunaliweka Jina Lake mbele ya maombi yetu. Na ndipo tunajua, kwa Neno Lake, ya kwamba utayajibu, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Hakuna haki yetu wenyewe, hakuna chochote tulicho nacho ambacho tungeweza kufanya; bali kwa neema pekee tunakuja, tukiomba katika Jina la Kristo.

³ Baba, kunaweza kuwa na wanaume na wanawake wengi hapa ndani, kwenye jengo hili usiku wa leo, ambao ni wenye dhambi. Ulikufa kwa ajili ya mwenye dhambi. Jalia huu uwe ndio usiku ambao Mungu atazungumza na mioyo yao na kuwaita kwa neema Yake, waingie katika Ufalme. Tujalie, Baba. Labda wamepoteza miaka mingi, wakizungukazunguka katika dhambi, lakini jalia hii iwe ndiyo saa.

⁴ Asante, Bwana, kwa ajili ya Billy Paul, usiku wa leo, maskini mvulana wangu mdogo, asiye na mama, anayetupwa huku na huku, asante, Bwana, kwa kumpa Roho Mtakatifu, kama hakikisho sasa, siku fulani tukufu tutaonana na mama tena, mambo yote ni sawa, yatakuwa sawa. Ee Mungu, jalia Malaika wamjulisha leo. Alilia hivyo wakati wa kifo chake, kwamba, “Mtumikie Mungu . . . siku moja Billy Paul atakuwa mtu mzima na kumpokea Roho Mtakatifu.” Maombi yamejibiwa. Mungu, mbariki mvulana huyo sasa. Jalia afuate nyayo za Bwana. Jinsi sauti yake ndogo ilivyokuwa ikitetemeka aliposema, “Baba, ndiyo kwanza nimpokee Roho Mtakatifu. Nina furaha sana.”

⁵ Mungu, jalia hilo liwe tukio la—la kila mtu ambaye hajazaliwa mara ya pili hapa usiku wa leo. Jalia wampokee Roho Mtakatifu usiku wa leo. Kama tumefanya dhambi

yoyote, utusamehe, Bwana. Waponye wagonjwa. Waimarishe waliovunjika mioyo.

⁶ Na sasa, Bwana, hata sijui nianzie wapi, kuzungumza usiku wa leo, lakini Wewe utatoa. Ninakuamini Wewe, na ninaomba ya kwamba utatupatia kitu ambacho kingewasaidia watu, kwa maana tunaomba katika Jina Lake. Amina.

⁷ Kwa usomaji mdogo tu wa Maandiko hapa, katika Isaya 35, ningependa kusoma. Maana, maneno yangu yatashindwa; Neno la Mungu halitashindwa kamwe. Kwa hiyo, hakuna—hakuna ibada inayokamilika bila kusoma Maandiko kwanza.

Nyika . . . mahali palipo ukiwa patafurahi; na jangwa litafurahi na kuchanua maua kama waridi.

Litachanua maua mengi, na kufurahi, naam, katika shangwe . . . kuimba: na utukufu utakuja Lebanoni . . . litapewa uzuri wa Karmeli na Sharoni, watauona utukufu wa BWANA, ukuu wa Mungu wetu.

Itieni nguvu mikono iliyo dhaifu, yafanyeni imara magoti yaliyolegea.

Waambie walio na . . . moyo wa hofu, Jipeni moyo, msiogope; tazama, Mungu wenu atakuja na kisasi, na Mungu pamoja na . . . malipo; atakuja na kuwaokoa ninyi.

. . . atafumbua, . . . masikio ya viziwi yatazibuliwa.

Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu, na ulimi wake aliye bubu utaimba: maana katika nyika maji yatabubujika, na vijito jangwani.

Na mchanga ung'ao mfano wa maji utakuwa ziwa la maji, na nchi yenye kiu itakuwa chemchemi za maji: . . . makao ya mbweha, ambapo kila mmoja alilala, patakuwa majani pamoja na mianzi na manyasi.

Na hapo patakuwa na njia kuu, na njia, . . . ya utakatifu; wasio safi hawatapita juu yake; bali itakuwa kwa ajili ya watu hao: wasafirio, wajapokuwa wajinga, hawatapotea katika njia hiyo.

Hapo hapatakuwa na simba, wala mnyama mkali ataenda . . . juu yake, hawataonekana hapo; bali waliokombolewa watakwenda katika njia hiyo:

Na hao waliokombolewa na BWANA watarudi, watafika Sayuni wakimba, na furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao: nao watapata kicheko na furaha, huzuni na kuugua zitakimbia.

⁸ Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusoma—kusomwa kwa Neno Lake. Ninataka kuzungumza usiku wa leo, Mungu akipenda, kwa dakika chache tu. Nitaangalia saa yangu hapa, ili nisiwaweke kwa muda mrefu sana usiku wa leo.

⁹ Baada ya ibada za juma hili, kujaribu kuwaonyesha watu kwamba hakuna haja ya kuwa na hofu. Kitu kibaya zaidi ibilisi anaweza kuweka juu yako ni hofu. Ikiwa hata ulikuwa na kansa na hukuogopa, na ukaamini kwamba Mungu angekuponya, usingekuwa katika hali mbaya sana. Mungu hushughulikia hilo; ikiwa ulikuwa mgonjwa, chochote kile, ikiwa hukuogopa. Kwa hiyo hofu ni mojawapo ya mambo mabaya sana ambayo Shetani anaweza kuweka juu ya mtu.

¹⁰ Sasa, juma hili nimejaribu kuthibitisha, kwa Maandiko, kwamba mtu aliyezaliwa mara ya pili katika Ufalme wa Mungu hana cha kuogopa. Uko salama kabisa, salama katika Yesu Kristo. “Wote alionipa Baba,” Yeye alisema, “watakuja Kwangu. Hakuna mtu anayeweza kuja isipokuwa Baba amwite. Baba hana budi kumwongoza hadi Kwangu; na yeye ajaye Kwangu, sitamtupa nje kamwe. Na yote. . . Hakuna mtu awezaye kuwapokonya kutoka katika mkono wa Baba Yangu; hakuna aliye mkuu kuliko Yeye. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa milele; hataingia katika hukumu, bali amepita kutoka Uzimani. . . kutoka mautini kuingia Uzimani. Aulaye mwili wangu na kuinywa Damu Yangu anao. . .” (Si “atakuwa na,” lakini “ana,” wakati uliopo.) “. . . Uzima wa milele, nami nitamfufua siku ya mwisho.”

¹¹ “Kwa hiyo msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata Siku ya Ukombozi wenu.” Haya basi. “Kutiwa muhuri hata Siku ya Ukombozi wenu.” Sio tu kutoka kwa uamsho mmoja hadi mwingine, bali hata Siku ya Ukombozi wenu.

¹² Jamani, jinsi Roho Mtakatifu alivyoingia asubuhi ya leo na kutubariki juu ya jambo hilo! Akatuweka hapa hadi saa saba na nusu, asubuhi ya leo, kuanzia yapata saa tatu na nusu. Jinsi alivyotubariki!

¹³ Sasa, usiku wa leo, nataka kuzungumza juu ya. . . Isaya alisema hapa, “Kutakuwa na njia kuu, na njia ya utakatifu.” Sasa nataka kuzungumza juu ya, “njia ya Mungu,” *Njia ya Mungu Iliyoandaliwa Kwa Ajili Yetu*.

¹⁴ Sasa, kama nilikuwa nikienda kwenye Jiji la New York, jambo bora kwangu kufanya si kujaribu kupata, kijiografia, mahali nilipo kisha nielekee kaskazini. Lakini njia bora ya kufanya ni kuchukua ramani na kuifuata hiyo ramani, (hiyo ni kweli?) barabara kuu. Nisipofanya hivyo, ninapata shida.

¹⁵ Hakuna njia za mkato katika Ufalme wa Mungu. Unajua, tunajaribu kupitia njia ya mkato, tunakuja hapa nje kwenye kidimbwi mahali fulani na kuingia matopeni. Na hivyo ndivyo tunavyofanya tunapotoka kwenye barabara kuu ya kale ya Mungu. Mungu alitengeneza njia ya miguu, njia.

¹⁶ Wana wa Israeli walipotoka katika nchi ya Misri, walifuata njia ya Mungu. Iliongoza hadi Bahari ya Shamu. Ajabu, kwamba Mungu angeielekeza njia Yake huko juu. Lakini njia yake ilipitia moja kwa moja baharini.

¹⁷ Kwa hiyo wakati ulipofika, na shindano la kuamua, nao Israeli wakasimama pale mbele ya bahari, njia ya Mungu iliongoza kupitia baharini. Kwa hiyo Mungu akatazama chini kupitia ile Nguzo ya Moto, bahari ikaogopa na kurudi nyuma, nao Israeli wakavuka kwenye nchi kavu. Njia ya Mungu ilipitia humo.

¹⁸ Kisha akapanda mpaka nyikani, kwenye chemchemi ya *Mara*, maji “machungu.” Si ni ajabu kwamba Mungu angewaongoza watoto Wake kupitia maji machungu? Lakini wote huifuata barabara. Lakini alipokuwa pale, tiba ya yale maji machungu ilikuwa imesimama ukingoni. Musa alikata mti na kuutupa ndani ya hayo maji, nayo yakageuka kuwa matamu tena.

Wengine kupitia majini, wengine kupitia mafuriko,

Wengine kupitia majaribu mazito, lakini wote kupitia Damu.

¹⁹ Hivyo ndivyo Mungu anavyowaongoza watoto Wake; njia ya Mungu, njia ya Mungu iliyoandaliwa. Kama wana wa Israeli wangelazimika kujaribu kukwepa, na kuzunguka, *huku* chini, wangeingia katika shida. Iliwabidi kufuata Wingu la Moto, ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza. Waliifuata Hiyo.

²⁰ Na laiti Kanisa, usiku wa leo, lingefuata tu ile Nguzo ya Moto, Roho Mtakatifu, mtafaulu kuingia Kanaani bila shaka yoyote. Mungu anayo njia, njia iliyowekwa.

²¹ Kuna njia mbili mtu anaweza kupitia, na hiyo ni njia yake au njia ya Mungu, na hiyo ni njia sahihi au njia mbaya. Na njia yako daima ni njia mbaya, na njia ya Mungu ni njia sahihi. Wala huwezi kuwa katika njia yako mwenyewe na njia ya Mungu kwa wakati mmoja, kwa hiyo huna budi kuiacha njia yako mwenyewe ili Mungu apate kuwa na njia Yake ndani yako. Hiyo ni kweli. Mungu hufanya njia iliyoandaliwa.

²² Mwanadamu daima alitaka kufanya njia yake mwenyewe. Katika bustani ya Edeni, Mungu alimwumba mtu hata haikumbidi kujisumbua kwa chochote. Mungu alimfanya kuwa mkamilifu, lakini mwanadamu alitaka njia yake mwenyewe. Alitaka kuharibu. Alitaka kujua. Na kisha mara tu alipoanguka... Tumepitia hilo juma hili, katika masomo ya Maandiko. Alijiundia mwenyewe dini. Hakumngojea Mungu amwandalie moja. Alijitengenezea moja mwenyewe, lakini aligundua ya kwamba dini yake, kifuniko chake, hakingefanya kazi. Huyu daima amekuwa ni mwanadamu. Anataka njia yake mwenyewe. Lakini Mungu alikuwa na njia. Kwa hiyo

mwanadamu akatengeneza majani ya mtini na kujivisha, yeye na mkewe, lakini, aliposhuka ili kukutana na Mungu, aligundua hayo hayangefaa kitu.

²³ Nami nawaambia, marafiki, kumekuwako na watu wengi, na wako usiku wa leo, wanaofikia mwisho wa safari, watakaogundua kwamba hiyo dini ndogo ya juujuu ambayo unashikilia haitafanya kazi. Hakuna kitu pungufu ya kuzaliwa mara ya pili kitakachofanya kazi. Yesu alisema, “Mtu asipozaliwa kwa maji na Roho, hataingia kamwe katika Ufalme.” Kamwe hataingia, haidhuru kama yeye ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, chochote alichokataingia mpaka azaliwe kwa maji na Roho. *Kuzaliwa* kunamaanisha yeye “amebadilishwa.” Hana budi kufa kabla hajazaliwa. Kwa hiyo huna budi kuifia nafsi yako, uzaliwe upya, tena, katika Kristo Yesu. Hiyo ni kweli.

²⁴ Sasa nataka mtambue, alijikuta akijaribu kutengeneza njia yake. Tulikuwa, asubuhi ya leo, na jinsi Kaini alivyojaribu kutengeneza njia yake. Alishuka na baadhi ya matofaa na peasi na mapichi na maboga, chochote kile, akayaweka madhabahuni na kusema, “Sasa hayo hapo, Bwana, nilijenga madhabahu. Nilijenga kanisa. Mimi ni mfuasi mzuri wa kanisa.” Mnaona? “Ninaenda kanisani kila siku. Nilikuja hapa, nikajenga madhabahu. Nikaweka dhambi juu yake. Sasa nitapiga magoti na kuomba. Na sasa, Bwana, nataka unipokee.” Lakini Mungu alimkataa.

²⁵ Na roho yule yule wa kale wa kidini anaishi moja kwa moja miongoni mwa kanisa siku hizi, jambo lile lile, wa kidini tu awezavyo kuwa, na hawajui zaidi kumhusu Mungu kama Mhotentoti angejua kuhusu hekaya za Misri. Unajua huo ndio ukweli. Roho za dini! Usifikiri kwamba Stalin ndiye mpinga-Kristo. Biblia ilisema, “Roho hizo mbili zingefanana sana, zingewadanganya walio Wateule kama yamkini.”

²⁶ Tunaona ya kwamba Yuda Iskariote alishuka moja kwa moja, na akatoka na kufurahi na kuhubiri Injili; akarudi, akipiga kelele na kupaza sauti, na kuwa na wakati mzuri pamoja na wanafunzi wengine. Mathayo Mtakatifu, mlango wa 10. Lakini aliwafuata wanafunzi moja kwa moja, hata hivyo, ibilisi aliyefanyika mwili, naye akaja moja kwa moja; kama vile Yesu alivyokuwa Mungu aliyefanyika mwili; yule Kaini na yule Habili kutoka bustani ya Edeni. Lakini ilipofikia wakati wake wa kupanda kwenda Pentekoste, na kupata zile baraka, alionyesha kile alichokata.

²⁷ Na unapoanza kuzungumza juu ya kuzaliwa mara ya pili, kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, mara tisa kati ya kila kumi, hizo roho zitaonyesha sifa zao, kile walicho. Watasema, “Hilo ni kundi la ulokole. Achana nao.” Ndugu, ni njia iliyowekwa na Mungu kwa mwanadamu kwa ajili ya siku hizi. Haleluya!

28 Tazama, Mungu daima ametengeneza njia iliyoandaliwa. Mungu yuko na wajibu wa kufanya njia. Mungu hufanya njia kwa ajili ya maumbile. Kwa nini tuna mafuriko haya makubwa kote nchini? Wanakata miti yote na mambo kama hayo, wanaacha yapelekwe na maji. Mnajenga bwawa hapa chini na kujaza chini ya mto; hayo hapo yanaenda, maji. Mnaharibu maumbile asilia. Mungu alikuwa na njia iliyowekwa. Hayo ndiyo yanayosababisha mafuriko. Chochote ambacho mwanadamu anaharibu, ambacho Mungu amekifanya kikamilike, nawe unakiharibu. Hiyo ni kweli.

29 Sasa, kama tu, kwa mfano, kama vile ma—mabata. Ninapenda kuwatazama mabata, kwenye misimu ninapoenda kuwinda mlimani. Ngingekuwa huko katika msimu wa majani kupukutika. Vema, huko mabata wote wanatoka Louisiana na kule chini, na chini kwenye vinamasi. Nao wanaenda kaskazini na kufanya makazi yao, wanatengeneza kiota na kuwalea maskini vifaranga wao. Ndipo hao jamaa wadogo wanainuka, labda kufikia Septemba, wakati huu wa mwaka, ama mwishoni mwa Septemba. Ndipo maskini bata mzee, maskini bata dume, kamwe hajawahi kutoka kwenye kidimbwi hicho. Yuko pale pale tu kwenye kidimbwi.

30 Baada ya muda jalidi inaruka juu ya mlima. Theluji kidogo inaanguka mle, na upepo baridi unavuma kupitia mlima huo. Maskini huyo bata anahisi huo. Sasa hajawahi kuwa popote ila kwenye hicho kidimbwi, hajapata umri wa mwaka mmoja bado. Anainua kichwa chake hewani, ule mlio mdogo, na kukimbia katikati ya kidimbwi, na kufanya “honki-honki,” kila bata kwenye hicho kidimbwi atamjia. Kila bata kwenye hicho kidimbwi anajua kwamba yeye amezaliwa kiongozi. Na maskini bata huyo atainuka kutoka kwenye kidimbwi hicho, bila dira wala chochote kile, na kwenda moja kwa moja hadi Louisiana, kwenye mashamba ya mpunga, awezavyo kwenda.

31 Inaonekana kama Wakristo wanapaswa kuwa na hisi ya bata, hata hivyo. Sivyo? Hiyo ni sawa. Sawa.

32 Kwa nini? Unasema, “Ni silika.” La, wanaenda kwa njia iliyoandaliwa na Mungu. Mungu aliwapa njia, silika ya kuwaongoza kule chini, nao wanaiamini.

33 Lakini, Mungu humpa mwanadamu Roho Mtakatifu, naye anamkataa, anayo njia yake mwenyewe. Lakini Mungu ana njia iliyoandaliwa kwa ajili yetu. Haleluya! Ninajisikia kidogo nimebarikiwa usiku wa leo, baada ya hili, na siku hizi chache usiku wa uamsho.

34 Angalia, huyo hapo. Naam, bwana. Maskini bata huyo atashuka huko.

35 Kisha nitawaambia jambo jingine. Ungeenda hapa kwenye gazeti; useme, “Kesho kutakuwa na hali nzuri ya hewa.” Nawe

ungeenda kuwinda na kuwaona hao sungura wakienda kukaa kwenye nyasi hizo. Usivutiwe na hayo magazeti.

³⁶ Mwangalie maskini huyo nguruwe akichukua makapi kutoka upande wa kaskazini wa kilima na kuyapeleka kule, upande wa kusini wa kilima, na kujifanyia ki—kitanda upande wa kusini wa hicho kilima. Anajua zaidi kulihusu kuliko wafafanuzi wote wa magazeti duniani. Kweli. Ana silika. Anazunguka upande wa kusini, kuukimbia upepo huo baridi wa kaskazini unaoshuka. Loo, jamani!

³⁷ Ikiwa nguruwe ana akili ya kutosha kujificha kutoka kwa upepo, vipi kuhusu wewe uliye na Roho Mtakatifu? Haleluya! Hiyo ni silika yako. Naam, bwana.

³⁸ Naye Mungu aliwapa silika. Ni njia ya Mungu iliyoandaliwa kwa ajili yao. Wanaishi katika njia ya Mungu iliyoandaliwa.

³⁹ Hebu chukua ua, linapokufa na kuingia ardhini. Sio mwisho wake; linaishi tena. Mungu aliliandalia njia, nalo linaiamini.

⁴⁰ Mungu daima amefanya njia iliyoandaliwa. Wakati mwingine haiongozi kwenye mambo ya kupendeza, wakati mwingine inapitia magumu, lakini ni njia ya Mungu iliyoandaliwa. Mungu huifanya, kwa vyovyote vile.

⁴¹ Wakati mmoja alikuwa na mtu katika njia ya Mungu iliyoandaliwa, ilimbidi aingie, kupitia tundu la simba, bali alipitia njia ya Mungu iliyoandaliwa. Mungu akamtoa nje tena. Haleluya!

⁴² Ninaweza kuwaona baadhi ya watoto wa Kiebrania wameketi kule Babeli asubuhi moja. Walikataa kusujudia sanamu. Hiyo ni kweli. Walisema, “Hatutafanya hivyo. Cheza muziki wote unaotaka, na kupiga buruji zako na baragumu, lakini hatutaisujudia sanamu yako.” Haleluya!

⁴³ Tupe akina Shadraka, Meshaki, na Abednego wengine, (naam, bwana) ambao hawatainamia mambo yako ya kilimwengu. Haitubidi kujisalimisha kwake. Mungu ametuweka huru, kwa Roho Mtakatifu. Haleluya! Naam, bwana.

⁴⁴ Sasa ninaweza kuona kule chini, asubuhi moja. Hebu—hebu tuelekeze kamera zetu huko chini kwa dakika moja, na tutazame tuone. Ninaweza kuwaona hao wavulana kule chini, asubuhi moja. Walisema, “Sasa tazama, mfalme alisema, ‘Kila mtu asiyesusujudu, tutamtupa katika tanuru ya moto.’”

⁴⁵ Nao wakaenda na kuomba kwa dhati, usiku mmoja. Kesho yake, sauti ilipokuja ya kwamba wangesujudu mbele ya hiyo sanamu, mbona, waliipa kisogo.

Kwa hiyo akaja huko, kasema, “Wavulana, mlifanya hivyo?”
“Naam.”

⁴⁶ “Vema, tutatia moto tanuru, moto mara saba kuliko ilivyowahi kuwa.”

47 Sasa si ajabu hiyo! Kulikuwa na ubao wa kuingilia uliowekwa hapo, ukielekeza hadi kwenye mdomo wa tanuru.

48 Kote katika Babeli kulikuwa kwekundu asubuhi hiyo, moto ukivuma. Ninaweza kumwona Mfalme Nebukadreza, kama mtu wa kisasa leo, ameketi kule nje na kusema, “Sasa tutachoma tu dini hiyo yote ya Roho Mtakatifu iwatoke watu hao.”

49 Loo, naam, usifikiri ibilisi hatakuchoma. Hakika atakuchoma. Lakini, kumbuka, Roho Mtakatifu Mwenyewe ni Moto.

50 Sasa, nataka mtazame, njia ya Mungu iliongoza moja kwa moja kwenye huo ubao wa kuingilia. Ninaweza kuwaona Shadraka, Meshaki, Abednego, wakitembea kwenye maandamano ya kifo. Ninaweza kumsikia Shadraka akisema, “Abednego, je, uliomba vya kutosha?”

“Naam,”

“Vema, basi.”

“Je, una uhakika kuwa uko katika njia ya Mungu?”

51 “Naam, bwana. Na Mungu alisema katika Neno Lake tuisujudia sanamu, wala hatutaisujudia. Mungu ana uwezo wa kutukomboa kutoka katika tanuru hii ya moto. Lakini asipotukomboa, inajalisha nini. Hatutaisujudia. Tunaenda kwa njia iliyoandaliwa na Mungu.”

52 Ninaweza kumsikia mtu akisema, “Je, una uhakika una njia Yake iliyoandaliwa?”

“Naam.” Haleluya!

53 Wengine wanasema, “Vema, hufikiri watu hao wote wanaweza kuwa sahihi, badala yako?”

54 “Hapana, bwana. Biblia ilisema hivyo, nasi tunadumu Nayo.” Moja kwa moja wanapanda ubao huo wa kuingilia. Naweza... Hilo joto ni... Hilo joto kali lilikuwa karibu... Liliwaua wale watu waliowaleta.

55 Walikuwa karibu tu kuingilia mle. Mungu alikuwa hajasema neno lolote. Bado wanatembea kwenye njia iliyoandaliwa. Wakatembea moja kwa moja hadi kwenye mdomo wa tanuru. Mara tu walipokuwa tayari kuingia kwenye ile tanuru ya moto... Mnajua, nina picha nyeusi ya kutisha hapa mbele yangu sasa hivi. Watu wanaojaribu kuishi waaminifu kwa Mungu, wanaotembea katika njia ya Mungu iliyoandaliwa; wakijitayarisha kuchomwa moto. Ni picha ya jinsi gani!

56 Angalia, wakati wote kuna jambo fulani linaloendelea hapa chini, kuna jambo fulani linaloendelea Kule juu, wakati ule ule. Hebu tuangalie Huko juu kidogo tuone kinachoendelea. Ninaweza kumwona amesimama pale, na mavazi Yake ya kifalme yamemzunguka. Haleluya! Ninaweza kuona, jambo la kwanza, kutoka upande wa kulia, Malaika mkubwa sana,

anayeitwa Mikaeli. Wana Mmoja kule juu. Je, mlijua hilo? Ninaweza kumsikia akikimbia kule kando Yake, akisema, “Bwana!” Ninaweza kumwona akichomoa upanga Wake kutoka kwenye ala Yake, namna *hii*, na kusema, “Je, umeitazama Babeli asubuhi ya leo? Kuna watu wanatembea kwenye njia ya Mungu iliyoandaliwa. Kuna watu walio tayari kutia muhuri ushuhuda wao asubuhi ya leo. Ndugu zetu wako karibu kabisa kuchomwa moto.” Naweza kumsikia akisema, “Ngoja nishuke huko! Nitabadilisha hiyo picha.” Naamini angeweza kuibadilisha; ninaamini.

⁵⁷ Ninaweza kumsikia akisema, “La, siwezi kukuruhusu kwenda. Gabrieli, umekuwa ninii, ama Mikaeli, umekuwa Malaika mzuri sana. Nenda, rudisha upanga wako, usimame wima hapo.”

⁵⁸ Huyu hapa Malaika mwingine anakuja, anaitwa Pakanga; huyafanya maji kuwa machungu. Huyu hapa anakuja, akasema, “Bwana, angalia kule chini. Nina mamlaka kamili juu ya maji. Uliyakabidhi kwangu katika yale maangamizi yaliyoitangulia ile gharika, nami nikaufagilia ulimwengu wote mbali, isipokuwa Nuhu na watu wake. Sasa,” akasema, “naomba nishuke kule na nitaifagilia mbali Babeli itoke kwenye ramani.”

⁵⁹ Ninaweza kumsikia akisema, “Pakanga, unaweza kulifanya, hiyo ni kweli, lakini siwezi kukuruhusu uende. Ni kazi inayohitaji Mtu-mkubwa.”

⁶⁰ Loo, ninaweza kumwona akiinuka, namna *hiyo*. Wako karibu kabisa kupiga hatua ya mwisho. Ninaweza kumwona akinyosha mkono pale na kusema, “Njoo hapa,” kwa radi kubwa inayoning’inia kule nyuma. Loo, jamani! Ilimtii.

⁶¹ Ninaweza kumwona, kumsikia akisema, “Upepo wa mashariki, kaskazini, magharibi, na kusini, njoni hapa muibebe radi hii. Nitawaendesha kama farasi. Nitaketi kwenye radi hii, asubuhi ya leo, kama gari la farasi. Ninashuka kwenda Babeli, Mwenyewe.” Haleluya!

⁶² Ninaweza kumwona akiinuka na kuishika radi ya zigizaga na kupasua anga kwayo, namna *hiyo*; wakati tu wao wanapiga hatua yao ya mwisho, wakitembea katika njia ya Mungu iliyoandaliwa. Na yapata wakati walipoingia mle, Yeye alipita kando ya Bahari ya Uzima na kuokota mtende, Naye alikuwa amesimama pale chini akiupepea upepo kutoka kwao. Haleluya! Daima Yeye yuko hapo wakati mtu atatembea kwa njia ya Mungu iliyoandaliwa. Naam, bwana.

⁶³ Wakati mmoja kulikuwa na mhubiri mzee “tapelibingwa”, mhubiri wa zamani wa utakatifu huko nyuma, zamani za kale, jina lake Nuhu. Alisema, “Mnajua, mvua itanyesha, dhoruba itakuja.”

⁶⁴ Ninaweza kuwasikia watu wakizunguka na kusema, “Aisee, mnamsikia yule mzee mtakatifu anayejifingirisha huko juu?”

Alisema, 'Mvua itanyesha.' Mbona, haikunyesha kamwe juu ya nchi. Na ati mvua itanyesha? Vipi, maji hayo yatatoka wapi? Vema, twende tuchukue sayansi tuone kama kuna maji yoyote huko juu. Mbona, hapana, hakuna maji huko juu. Kuna nini? Huyu mhubiri mzee amerukwa na akili."

⁶⁵ Lakini Mungu alisema hivyo! Mungu alisema, "Tengeneza safina, Nuhu, kwa ajili ya wokovu wa nyumba yako, kwa wokovu wa watu." Naye Nuhu alikuwa na akili ya kutosha kufanya hilo. Ni hayo tu. Alikuwa na kutengeneza safina.

⁶⁶ Basi siku moja, ninawasikia baadhi yao chini pembeni, wakizungumza, huko kwenye kona ya biashara. Baadhi yao wanasema, "Aisee, vipi kuhusu ile hadithi ya mvua huko juu, maskini yule mhubiri tapelibingwa akisema kwamba itanyesha huko juu? Je, mumewahi kusikia jambo kama hilo? Naye anafikiri yuko katika njia ya Mungu iliyoandaliwa." Alikuwa. Amina.

⁶⁷ Muda si muda mnajua, kukaja ngurumo na radi. Ninaweza kumwona maskini ngamia mama, mzee mkubwa akitoka kule nje, akiangalia juu na kusema, "Baba Ngamia, unasikia hiyo ilikuwa ni nini? Hiyo ilikuwa ni ngurumo. Hivyo ndivyo alivyosema Nuhu. Twende kwenye safina." Hao wakashuka chini ya kilima. Na hawa hapa wanakuja baba farasi na mama farasi, na wawili-wawili wa hao wengine wote, moja kwa moja kwenye safina, mmoja baada ya mwingine. Mungu akaufunga mlango, akaleta mvua. Nuhu alikuwa katika njia ya Mungu iliyoandaliwa.

⁶⁸ Baadhi yao wakapanda juu ya magogo, wakasema, "Nitaelea kote." Lakini nitawaambia, wakati dhoruba zilipoanza kuvuma, safina ilipaa juu. Haleluya! Kwa nini? Walikuwa katika njia ya Mungu iliyoandaliwa. Mungu daima atawabariki watu ambao watatembea katika njia ambayo Yeye ameandaa. Kamwe hakuandaa gogo. Hakuandaa *hii*. Aliandaa safina.

⁶⁹ Na, leo, ndugu na dada yangu, kuna njia iliyoandaliwa kwa ajili ya wanaume na wanawake, hiyo ni kwa njia ya Yesu Kristo Mwana wa Mungu, aliyekufa pale Kalvari, na kupitia Damu Yake tuna ondoleo la dhambi; na tunaweza kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, kama kibali cha Mungu, kwamba ametukubali katika Mwanawe, Kristo Yesu. Salama salimini! Haleluya!

⁷⁰ Mtaniita mtakatifu anayejifingirisha, kwa vyovyote vile, kwa hiyo afadhali muanze. Vema. Najisikia vizuri sana. Vema.

⁷¹ Je, unaamini Hilo? Hiyo ndiyo njia ya Mungu na njia pekee. Si njia ya Methodisti, si njia ya Baptisti, si ya Presbiteri, si ya Pentekoste. Ni njia ya Kristo. Kristo ndiye njia ya Mungu iliyoandaliwa. Yeye ni dhabihu ya Mungu iliyotolewa. Yeye ni Yehova-Rafa. Yeye ni Yehova-Yire. Yeye ni Yehova-Manase.

⁷² Ibrahimu alipomtoa Isaka, alipaita mahali pale, *Yehova-Yire*, "Bwana atajitolea Mwenyewe dhabihu." Na hiyo hapo,

Mwana wa Mungu. Amina. Mungu daima hufanya njia ya kuepukia. Naam, bwana.

⁷³ Wakati mmoja kulikuwa na mhubiri mzee kule chini akihubiri, jina lake Elisha. Alipanda pale na akaitazama nchi nzima, akasema, “Ninakwambia, ndiyo mbaya kuliko zote nilizowahi kuona.”

⁷⁴ Maskini mfalme kule chini alienda na kumwoa maskini Yezebeli aliyejipaka rangi, rangi ya kutosha usoni mwake kufanya... Mwanamke pekee katika Biblia ambaye aliwahi kupaka uso wake rangi. Basi mnajua kile Mungu alimchomfanyia? Mungu alimlisha kwa mbwa. Huyu ndiye pekee ninayemjua.

⁷⁵ Ukimwona mwanamke mwenye rangi nyingi usoni mwake, unajua unaweza kumwitaje? Sema, “Habari, Binti Nyama ya Mbwa!” Hivyo ndivyo alivyo, kama nyama ya mbwa. Loo, jamani! Sikilizeni, ndugu, nimerudi hivi punde tu kutoka Afrika. Kitu hicho kinatokana na asili ya ukafiri. Makafiri hujipaka rangi.

⁷⁶ Loo, ndugu, wakati mwanamume ama mwanamke anapopatana na Mungu, huna haja kuwaambia jambo hilo; wanaona aibu, wenyewe. Haleluya! Hiyo ni kweli.

⁷⁷ “Jamani, muda si muda mnajua, atawafanya Waisraeli hawa wote wafanye hivyo.” Eliya alisema, “Bwana, zifunge mbingu. Fanya jambo kuhusu hilo.”

⁷⁸ Mungu alinena chini na kusema, “Sasa, Eliya, hebu nikwambie utakalofanya. Shuka ukaseme na Ahabu.”

⁷⁹ Na huyu hapa mhubiri mzee anakuja, akishuka kupitia pale, akiwa amejizungushia kipande kikubwa cha ngozi ya kondoo namna hiyo, uso umefunikwa na masharubu kama mdudu manyoya. Akaenda mbele ya mfalme na kusema, “Umande hata hautaita... au hautaanguka ila kwa neno langu.” Haleluya! Alikuwa katika njia ya Mungu iliyoandaliwa. Naam, bwana.

⁸⁰ “Aha, ondoka hapa, ewe mlokole. Vema, tunajua tunachofanya.”

⁸¹ Mzee Eliya akasema, “Bwana, nifanye nini? Uliwawekea wengine njia. Nimefanya hivyo.”

Kasema, “Nenda pale kando ya kijito Kerithi ukaketi chini.”

⁸² “Sawa, mahali pabaya sana, lakini nitapanda niketi chini. Ulisema, ‘Panda huko juu.’ Njia Yako ikielekeza kule, nitakwenda kule.”

⁸³ Akapanda na kuketi chini. Kasema, “Sasa, Bwana, nitafanya nini hapa?”

“Keti hapo. Ketu tu hapo.”

⁸⁴ Na muda si muda mwajua, akaanza kushikwa na njaa. Akasema, “Bwana, kidogo ninashikwa na njaa.” Na huyu hapa kunguru akaja.

⁸⁵ Baadhi yao wakasema, “Mwangalieni yule mhubiri mzee anayejifingirisha ameketi kule juu kilimani. Mbona, si wazimu yule! Vema, jamaa yule, anayeketi kule kwenye jua, atakufa. Mbona, yeye ni mloko.”

⁸⁶ Na muda si muda mwajua, maji yote yakakauka. Hakuna maji ya kunywa, huko chini n—nchini. Lakini kila mara Eliya alipotaka kunywa, aliinama tu kwenye kijito cha Kerithi na kunywa. Ndipo alipoona njaa, huyu hapa kunguru anakuja, akiwa na sambusa mdomoni mwake, akasema, “Haya basi, Eliya.”

⁸⁷ Unasema, “Huyo kunguru alipata wapi...? Unamaanisha unaamini hilo, Ndugu Branham?” Naam, bwana. Naam, bwana. “Unamaanisha kwamba kunguru alimletea Eliya chakula kwa muda wa miaka mitatu na miezi sita?” Ninaamini hilo. Wasema, “Kwani alikipata wapi?” Sijui. Kitu pekee ninachojua, kunguru alikipata mahali fulani, akamletea Eliya, Eliya alikila na kuishi miaka mitatu na miezi sita kwa hicho. Hiyo ni kweli. Ninaamini.

⁸⁸ Hilo ni jambo lile lile kuhusu... Unasema, “Ni nini kinachokufurahisha hivyo? Ni nini kinachokufanya uutikise mkono wako?” Sijui. Kitu pekee nijuacho, Kalvari ilililipia, Biblia ikalifundisha, Roho Mtakatifu akalileta, nikalipata. Haleluya! Hata sijui limetoka wapi, lakini nimelipata. Haleluya! Hiyo ni kweli. Siwezi kukwambia linatoka wapi, lakini limefika hapa. Loo, jamani! Hufanya koti lako likutoshee vizuri zaidi. Hakika. *Haleluya!* Usisisimkwe. Hilo linamaanisha “msifu Mungu wetu.” *Amina!* Hiyo inamaanisha “na iwe hivyo.” Loo, jamani! Hakika, ndivyo ilivyo. Sijui... .

⁸⁹ Nao walisema alikuwa na kichaa, ameketi pale juu? Jamani! Ukaja... Ukaja wakati wa kula, huyu hapa mpagazi mweusi anakuja, akasema, “Haya basi, Eliya. Hiki hapa kifungua kinywa chako.” Mbona, alikuwa bora kuliko nusu ya watu hapa ndani usiku wa leo. Nawazia hakuna wengi humu ndani usiku wa leo walio na watumishi weusi. Lakini alikuwa na watumishi weusi, baadhi ya kunguru wakimletea chakula kwa kila mlo. Haleluya! Utukufu! Mungu alikuwa na chumba cha kulia chakula mahali fulani; alikitayarisha, akakipika, akampelekea. Haleluya! Mungu yuyo huyo anaishi na kutawala leo.

⁹⁰ Alikaa katika njia Yake iliyoandaliwa. Mungu alisema, “Nenda huko ukaketi,” kwa hiyo akafanya hivyo. Hayo tu ndiyo aliyojua kufanya. Unafikiri nini kuhusu hilo, unaamini kuwa ni kweli? Hiyo ni kweli. Amina. Naam, bwana.

⁹¹ Msichana mdogo alikuwa akishuka barabarani siku moja, naye akasema... Hatimaye, mmoja akasema... “Loo, haleluya! Haleluya!” Ndiyo kwanza ampokee Roho Mtakatifu.

92 Kwa hiyo kulikuwa na maskini kafiri aliyeketi pembeni, akasema, “Ni kitu gani kinakufurahisha sana hivi, msichana?”

93 Kasema, “Loo, Yesu ndio kwanza aniokoe na kunijaza na Roho Mtakatifu.” Kasema, “Nina furaha sana.”

Kasema, “Angalia, ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako?”

Kasema, “Biblia yangu.”

Kasema, “Je, unaiamini Hiyo?”

“Hakika.”

Kasema, “Je, unaiamini yote?”

“Yote.”

Kasema, “Je, unaamini hadithi hiyo kuhusu Yona?”

“Naam.”

94 Kasema, “Je, unaamini kwamba kweli nyangumi huyo alimmeza huyo mtu?”

“Naam, bwana. Ninaiamini.”

95 Kasema, “Utathibitishaje jambo hilo kwa njia nyingine yoyote isipokuwa imani?”

96 Akasema, “Vema, nitakapofika Mbinguni nitamwuliza tu Ndugu Yona.”

97 Huyo kafiri akamwambia, kasema, “Vipi kama Ndugu Yona hayuko Mbinguni?”

98 Kasema, “Basi itakubidi umwulize wewe.” Haleluya! Nafasi moja tu iliyobaki kwake, hiyo ni kuzimu.

99 Ukiikataa njia ya Mungu, huna budi kwenda kuzimuni. Huna budi kwenda. Ndiyo njia nyingine ya pekee. Kwa hivyo uko kwenye njia moja au nyingine. Amina. Vema.

100 Ninaweza kumwona kule chini, ameketi kule juu na kunguru wakimletea chakula.

101 Akarudi kule chini. Akashuka mlimani, siku moja. Naye Mungu akasema, “Sasa kidimbwi kimekauka. Nataka ushuke huko chini kwa nyumba ya mjane.” Ni mahali pa namna gani kwa mhubiri kwenda! Mungu alimwambia aende. Hiyo ilikuwa ndiyo njia iliyoandaliwa. Akashuka kule chini. Wala yeye hakuwa Mwisraeli, pia. La, hakuwa. Naye akarudi pale... Naye akashuka mlimani.

102 Basi aliposhuka mlimani, alikutana na mjane mzee amesimama uani, akivunja kijiti chake pamoja. Kasema, “Ingia ndani unipe chakula, na uniletee maji ninywe.”

103 Akasema, “Kama Bwana aishivyo, na nafsi yako haifi kamwe, nina unga wa kutosha tu nyumbani kumpikia mwanangu keki moja ndogo. Ninachukua vijiti viwili ili nikapike keki hii, ndipo mimi na yeye tule kisha tufe.”

104 Kasema, “Nenda uniletee maji kidogo, kwanza, na uniokee keki uniletee.” Haleluya!

105 Atafanya nini? Hiyo hapo njia ya Mungu iliyoandaliwa. “Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki Yake yote.”

106 Unasema, “Ndugu Bill, mama yangu alitoroka nyumbani. Mume wangu hataishi nami.”

107 “Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki Yake,” haleluya, “mambo haya mengine yote yataongezwa.” Hiyo ni kweli.

108 “Nitafanyaje jambo hilo, Ndugu Bill?” Endelea tu na kulifanya. Yesu alisema, “Unifuata.” Hiyo ni kweli. Elekeza jicho lako mahali pamoja. Vema.

109 Na muda si muda mwajua, anaingia ndani, anachukua vijiti hivi viwili na kuvivunja. Mnajua jinsi njia ya kale ya Kihindi ya kuvunja kijiti? Hiyo ilikuwa ni msalaba, bila shaka. Na katika msalaba, wanauchoma moja kwa moja katikati. Hapo ndipo moto ulipowashwa, jiko hilo la keki nyembamba.

110 Akatoa keki na kumpa mhubiri, naye akasimama pale na kula. Kasema, “Sasa rudi na ujipikie moja yako na mvu- . . . mwanao. Kwa maana, BWANA ASEMA HIVI, lile pipa halitapungua, wala ile chupa kukauka, hata siku ile Mungu atakapoleta mvua juu ya nchi.” Haleluya!

111 Ati nini? Kwa sababu alitafuta Ufalme wa Mungu kwanza, kwa maana alitembea katika njia ya Mungu iliyoandaliwa, Mungu alimtuza. Je, unaamini hilo? Naam, bwana.

112 Kulikuwa na mwanamke wakati mmoja aliyepoteza kaka yake. Jina lake lilikuwa Lazaro. Loo, alikuwa mvulana mzuri; alichukia kumwachilia. Naye alikufa. Akaagizia mchungaji wake aitwe, ama mwinjilisti, ambaye alikuwa ni Yesu. Alikuwa ametoka kanisani, na alikuwa ameacha vyote walivyokuwa navyo. Naye akaagizia Yesu aje, aombe, Naye akaendelea mbele tu. Akaagizia tena, Naye akaendelea mbele tu. Akasema, “Sifanyi chochote mpaka Baba anionyeshe.” Baba alikuwa tayari amemwonyesha Lazaro alikuwa anaenda kufa.

113 Akaja, baada ya kitambo kidogo, baada ya siku tatu ama nne hivi. Akasema, “Lazaro amekufa, na kwa ajili yenu ninafurahi kwamba sikuwapo. Lakini naenda kumwamsha.”

114 Kwa hiyo basi alisikia Yesu anakuja, hivyo akatoka kwenda kumlaki.

115 Hiyo ilikuwa njia iliyoandaliwa na Mungu, nenda ukamlaki Yesu. Hiyo ni kweli, sikuzote. Ukiwa na huzuni nyumbani kwako, nenda ukamlaki Yesu. Ukiwa na magonjwa nyumbani kwako, nenda ukamlaki Yesu. Ukiwa na maumivu ya moyo nyumbani kwako, nenda ukamlaki Yesu. Haleluya! Ukiwa na haja ya kitu chochote, nenda ukamlaki Yesu. Nenda ukamlaki.

Ana suluhisho lote, kila kitu pale; hana suluhisho, anayo tiba. Amina.

Basi akaenda kumlaki, akaanguka miguuni Pake.

¹¹⁶ Naye alikuwa amesoma hadithi, wakati mmoja, ambapo kulikuwa na mwanamke huko nyuma kabisa katika Biblia, na Mshunami. Alimjali sana mhubiri aliyeitwa Elisha. Kwa hiyo akatengeneza chumba kidogo kando ya nyumba yake pale, akaweka kitanda na mshumaa na stuli, kadhalika. Naye Elisha akaja na akaona wema huu wote aliokuwa amemtendea mhubiri, akalipa zaka zake na kila kitu, mwajua. Hivyo akasema, “Nenda ukaulize, tuone tunachoweza kufanya, kama nitaenda kuzugumza na mfalme au jemadari mkuu.”

¹¹⁷ Akasema, “Ninakaa na watu wangu na kila kitu kiko sawa.”

Kasema, “Vema, nenda kamwulize nifanye nini.” Gehazi akasema, “Yeye ni tasa. Hana watoto.”

¹¹⁸ Kasema, “Nenda umwambie, BWANA ASEMA HIVI, ‘Panapo wakati huu mwakani, kwa muhula wake, kwamba atamkumbatia mtoto wa kiume.’” Naye akamkumbatia.

¹¹⁹ Mtoto akafikia kwenye umri wa miaka kumi na mmoja au kumi na miwili. Siku moja, yapata saa sita mchana, alikuwa nje kondeni pamoja na baba yake, naamini alishikwa na ugonjwa wa jua kali. Akaanza kupiga kelele, “Kichwa changu! Kichwa changu!” Akamtuma mmoja wa watumishi pamoja na huyo mtoto mchanga, mvulana. Akamweka kwenye mapaja ya mama yake. Saa sita mchana akafa.

¹²⁰ Ni mahali pazuri jinsi gani! Akamchukua na kumlaza juu ya kitanda cha yule mhubiri, ambapo nabii alikuwa amelala. Mahali pazuri pa kwenda. Akalazwa moja kwa moja kwenye kitanda cha mhubiri.

¹²¹ Akasema, “Nitandikie nyumbu sasa na uende mbele, wala usisimamishe mwendo mpaka nikwambie.”

¹²² Napenda hilo. Songa mbele wala usisimame! Mwendeshe tu. Hiyo ni kweli.

¹²³ Shida yake ni kwamba, tunasimama na kuzungumza na watu wengi kupita kiasi. Tunasimama kwa karamu nyingi sana za kijamii. Tuna kushona-na-kushonelea kwingi, na kuunda chama cha ushonaji, mwajua, kushona-na-kushonelea na kuzungumza juu ya Binti *Nanii*. *Nyinyi* mnajua jinsi ilivyo. Mambo haya yote mbalimbali yanakuja kanisani. Wakati, unapaswa kutupa maji hayo yote machafu, na kuwa na uamsho wa mtindo wa kale, uliotumwa na Mungu; kuomba kwa bidii, mpaka umerudi, Mbingu zimeshuka na Roho Mtakatifu anakuja kama upepo wa nguvu ukienda kasi na kupajaza mahali hapo na watu. Amina. Huo ndio tunaohitaji.

Akasema, “Usisimame.”

124 Naye mumewe akasema, “Mtu huyo hayuko Karmeli.” Kasema, “Huu sio mwandamo wa mwezi wala sabato.”

125 Akasema, “Yote ni shwari.” Alitaka kufika kwa nabii. Kwa hiyo aliendelea moja kwa moja.

126 Elisha akatazama nje na kusema, “Huyu hapa yule Mshunami anakuja. Ana tatizo; sijui ni nini.”

127 Akaja mbio. Naye akasema, “Je, wewe na mume wako, mtoto wako hamjambo?”

128 Akasema, “Hatujambo.” Napenda hilo. Alikuwa amepitia njia ya Mungu iliyoandaliwa. Kasema, “Kila kitu kiko sawa sasa.” Ndipo akaanza kulifunua.

129 Akamwambia Eliya, akasema, “Nenda, chukua fimbo yangu ukaiweke...” Au, akamwambia Gehazi, “Nenda kachukue fimbo yangu ukaiweke juu ya huyo mtoto.”

130 Lakini mama akasema, “Sitakuacha.” Kwa hiyo nabii akarudi, akaomba, akatembea huku na huku chumbani, akaulaza mwili wake juu ya yule mtoto aliyekufa, naye akawa hai.

131 Yule mwanamke, Martha, alijua kwamba yule Mshunami alitambua kwamba Mungu alikuwa ndani ya nabii Wake. Na kama Mungu alikuwa ndani ya nabii Wake, hakika Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe. Kwa hiyo kama angeweza kufika kwa Yesu, angekuwa na suluhisho. Kwa hiyo akakimbia na kuanguka chini mbele Yake. Akasema, “Bwana, ikiwa...” Hivyo ndivyo alivyokuwa. “Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini, hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atalifanya.” Loo, napenda hilo. “Hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atalifanya.”

132 Hilo ni zuri usiku wa leo. Unasema, “Mimi ni mwenye dhambi, Ndugu Branham.” Hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atalifanya. “Unihurumie, mwenye dhambi,” Naye atalifanya. Ikiwa wewe ni mgonjwa, “Unirehemu, Bwana,” Naye atalifanya hata sasa. Unasema, “Daktari alinikatia tamaa; lakini, hata sasa, Bwana! Sijatembea kwa miaka mitano; lakini, hata sasa, Bwana! Sijasikia chochote, kwani sijui ni lini; hata sasa, Bwana. Sijasema neno lolote, siwezi kukwambia ni lini, lakini hata sasa, Bwana.” Lolote utakalomwomba Mungu, Naye ameketi mkono wa kuume wa Baba, akifanya maombezi juu ya maungamo yenu. Haleluya!

Kasema, “Hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atalifanya.”

133 Akaunyoosha mwili Wake mdogo, akasema, “Ndugu yako atafufuka tena.

134 Kasema, “Loo, naam, Bwana, katika ufufuo wa kiama katika siku ya mwisho, atafufuka tena.”

Akasema, “Mimi ndimi huo ufufuo na Uzima.” Loo, jamani!

¹³⁵ Biblia ilisema, “Hakuna uzuri wa kumtazama, maskini Jamaa mdogo anayeonekana dhaifu.” Lakini akasema... Alipojinyosha, kulikuwako na Mungu.

¹³⁶ Akasema, “Sasa ndugu yako atafufuka tena.” Kasema, “Mimi ndimi ufufuo na Uzima,” asema Mungu. “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Kila aishiye na kuniadini Mimi hatakufa hata milele. Je, unasadiki haya?”

¹³⁷ Akasema, “Naam, Bwana. Mimi mimesadiki kwamba Wewe ndiwe Mwana wa Mungu ajaye ulimwenguni.”

¹³⁸ Kasema, “Mmemweka wapi?” Huyu hapa anaelekea kaburini. Yesu akalia machozi.

¹³⁹ Mwanamke mmoja aliniambia muda si mrefu uliopita... mwanamke mzuri sana, Mwanasayansi ya Kikristo ambaye hakuamini kwamba Yesu alikuwa... alikuwa na Uungu. Aliamini Yeye alikuwa ni nabii. Aliamini kwamba Yeye alikuwa mtu mwema, lakini hakuwa Yeye hakuzaliwa na bikira. Wanakataa kuzaliwa na bikira.

¹⁴⁰ Isitoshe, bali uchunguzi ulionyesha kwamba asilimia themanini na tano ya wahubiri wa Kiprotetanti wa Marekani wanadai kwamba kuzaliwa na bikira kulikuwa ni bandia. Kweli. Ningeweza kufanya hivyo kwa urahisi, ningeweza kufikiria hilo kwa urahisi kwa jinsi unavyoliishia. Hiyo ni kweli kabisa, wanaamini kuwa ni bandia. Na asilimia kubwa kuliko hiyo hawakuamini kwamba Yesu angerudi tena akionekana. Si ajabu tunahitaji uamsho!

¹⁴¹ Ndugu, sikiliza hapa. Unasikia mengi sana kuhusu uamsho, siku hizi. Hatukuwahi kuwa na uamsho.

¹⁴² Nilimfuata mtu mwingine, hapa si muda mrefu uliopita, ambapo wanazungumza mengi kuhusu haya. Kasema, “Alikwenda katika mji mmoja akapata waongofo elfu tano.” Tukafuatilia moja kwa moja nyuma yake, (si mimi) kundi la wahudumu, na wakachukua zile kadi na kuwafuatilia nyuma tena, na katika muda wa siku thelathini hawakuweza kupata thelathini waliodai kuokolewa. Unajua ninachofikiria? Nafikiri ni kusadikishwa badala ya kuongoka, wakati mtu anapozaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu.

¹⁴³ Tunachohitaji leo si mkutano mrefu, bali uamsho wa mtindo wa kale, wa Roho Mtakatifu, uliotumwa na Mungu; dini ya zamani za kale, ya anga ya bluu, inayoua dhambi, iliyooshwa kwa Damu. Amina. Hukufanya uchukue vyombo hivyo vya tairi, na kufanya toba. Hiyo ni kweli.

¹⁴⁴ Akasema, kisha akasema, “Vema, angalia hapa, Ndugu Branham, ninaweza kukuthibitishia kwamba Yeye hakuwa kitu ila mwanadamu.”

145 Nikasema, “Endelea. Kama unaweza kunithibitishia ya kwamba Yeye hakuwa Mungu, basi nitalikubali.”

146 Akasema, “La, Yeye hakuwa Mungu. Alikuwa mwanadamu tu. Nami ninaweza kuthibitisha hilo kwa Biblia, ya kwamba Yeye alikuwa mwanadamu tu.”

147 Nikasema, “Kama unaweza kulithibitisha kwa Biblia, basi nitalikubali.” Akasema, “Uko tayari?” Nikasema, “Niko tayari.”

148 Akasema, “Aliposhuka, katika Yohana Mtakatifu 11, alipoenda kwenye kaburi la Lazaro, alilia machozi.”

Nikasema, “Hiyo ina uhusiano gani nalo?”

149 Kasema, “Mbona, hilo lilithibitisha kuwa Yeye hakuwa kitu ila mwanadamu, alikuwa akilia.”

150 Nikasema, “Angalia hapa, mama. Yeye alikuwa mwanadamu, kweli, lakini alikuwa zaidi ya mwanadamu. Alikuwa Mungu-Mtu.”

151 Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Naam, bwana. Alikuwa kufanya mapenzi ya Baba. Alitembelea njia iliyowekwa na Mungu. Hakutazama kamwe kulia wala kushoto; alifanya yale Mungu aliyosema yafanywe. Alikuwa njia ya Mungu iliyoandaliwa.

152 Na akiwa njiani kwenda kwa Lazaro, alilia. Alikuwa mwanadamu alipokuwa akilia.

153 Lakini aliposimama pale kando ya kaburi, ambamo mtu alikuwa amekufa siku nne; na mabuu yanayotambaa yakiingia na kutoka mwilini mwake, na harufu mbaya kote humo; wakati aliposema, “Lazaro, njoo huku,” naye mtu aliyekuwa amekufa siku nne, akasimama kwa miguu yake na kuishi tena. Huyu alikuwa zaidi ya mwanadamu. Haleluya! Naam, bwana. Yeye alikuwa ni mwanadamu akilia, bali alikuwa Mungu katika huo ufufuo.

154 Yeye alikuwa ni mwanadamu aliposhuka kutoka mlimani, usiku ule, akiwa na njaa, akitazama pande zote, juu ya miti, akitafuta chakula. Alikuwa mwanadamu wakati alipokuwa na njaa.

155 Lakini alipochukua biskuti tano na vipande viwili vya samaki, na kuwalisha watu elfu tano, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Huyu alikuwa ni Mungu katika mwili. Haleluya!

156 Yeye alikuwa ni mwanadamu alipolala kwenye ile mashua usiku ule, wakati nguvu zilikuwa zimetoka kwenye vazi Lake; mpaka akadhoofika sana mpaka jioni, huku bahari kuu ikivuma, pepo elfu kumi wa baharini waliapa kuwa watamzamisha usiku huo; wakati maskini ile mashua ya kale, ikirushwarushwa huku na huko, kama kizibo cha chupa kwenye bahari kuu. Ninajua Yeye alikuwa mwanadamu alipokuwa amelala pale, usingizi, lakini waliposema, “Si kitu Kwako kwamba tunaangamia?”

157 Akaweka mguu Wake kwenye demani ya hiyo mashua, akasema, “Amani, tulia,” kukawa shwari. Huyu alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Haleluya! Huyu alikuwa ni Mungu wangu. Haleluya! Kweli, alikuwa; naam, kweli, ndiye.

158 Alikuwa mwanadamu alipokuwa amening’nia pale Kalvari, walipompa heshima kuu kuliko zote walizopata kumpa. Waliposema, “Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa Mwenyewe.” Ni sifa ya ajabu jinsi gani, au pongezi, walizompa. Kama aliokoa hawa wengine na Yeye Mwenyewe, hangeweza kuwaokoa wengine. Kwa hiyo, ilimbidi kujitua Mwenyewe, kusudi awaokoe wengine. Alikuwa mwanadamu alipolia apate rehema, aliposema, “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?” Alikufa kama mwanadamu. Naam.

159 Lakini alipofufuka kwenye asubuhi ya Pasaka, alithibitisha Yeye alikuwa ni Mungu. Si ajabu nabii alisema:

Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:
Siku moja yuaja—loo, siku yenye utukufu!

160 Haleluya! Nampenda. Nanyi je? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Tembea katika njia ya Mungu iliyoandaliwa.

161 Ninaweza kuwaona baadhi ya mamajusi, wakati mmoja, wakienda kwenye kuzaliwa Kwake, kumwabudu. Ninaweza kuwaona wote wakijiandaa. Wanafunga ngamia wao.

162 Ninaweza kumwona Jim Jones na wengine wote, na John Doe, wakipakia. Ninaweza kuwaona wakiweka meza hizi za kadi, zikiwa zimewekwa hapa kando namna *hiyo*, nao wakaweka kila kitu kingine, nao walikuwa wanaenda kumwabudu Yesu. Walikuja kugundua, walipofika huko, waliaamua maskini hao ngamia wasingeweza kutembea.

163 Hiyo ndiyo shida tu ya kanisa siku hizi. Mmebeba ulimwengu mwingi sana pamoja nalo, unawarudisha nyuma. Hiyo ni kweli.

164 Ninaweza kumwona akianza namna hiyo, na hao wote. Wakafika kando ya mlima kule, hawawezi hata kupita, maana, “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, na watakaoipata ni wachache.” Naam, bwana.

165 Ninaweza kumwona mzee mmoja akipakia mizigo, alikuwa akijifanya kuwa mwepesi, maana, “Ninapakia mizigo, kwenda Mbinguni.”

166 Ndugu, sipakii mizigo, kwenda Mbinguni. Ninafungua mizigo, niende Mbinguni. Haleluya! Kisha, Unyakuo, katilia mbali kila kitu. Biblia ilisema, “Na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi, ili tupige mbio hizi kwa saburi.”

167 Ninaweza kumwona maskini huyo jamaa mzee akienda, mnaona. Ninaweza kumwona mke wake karibu, kasema, “John, kuna nini, jamani? Unaenda wapi?”

Kasema, “Ninaenda kumwabudu Bwana.”

“Unajuaje kuwa unaenda?”

“Vema, ninaenda.”

168 “Vema, huna hata dira. Huna hata leseni yako ya huduma. Kwani una shida gani? Je, watakupokea? Ati unaenda kumwabudu Bwana?”

“Naam.”

“Chukua dira yako.”

“Hapana, siihitaji.”

“Ati huihitaji? Utafikaje huko?”

169 Ninaweza kumwona akielekeza kwenye Nyota ya asubuhi, akisema, “Ninaenda kwa njia ya Mungu iliyoandaliwa.” Amina. Mungu alitoa Nyota, iwaongoze wale mamajusi. Hawakuhitaji dira. Walihitaji njia ya Mungu iliyoandaliwa, ile Nyota. Utukufu!

170 Na Mungu yeye yule aliyewaongoza wale mamajusi kwa Kristo, kwa ile Nyota, yuko hapa usiku wa leo katika umbo la Roho Mtakatifu, kukuongoza kwa Kristo, Kuzaliwa upya, ubatizo wa Roho Mtakatifu, ambao ni njia ya Mungu iliyoandaliwa. “Mtu asipozaliwa kwa maji na Roho, hata hatauona Ufalme wa Mungu.” Wanaume kwa wanawake, mmempokea?

171 Muda wangu umekwisha. Loo, jamani, ninajisikia tu kuingia katika hilo. Niingize mkono wangu kwenye mifuko ya suruali yangu, na kuhubiri kama maskini mhubiri mzee wa mtindo wa kale. Kwa nini? Nalipenda. “Jamani, napenda kula aiskrimu,” lakini unapaswa kuwa na nyama ya nguruwe na maharagwe ili kuzishikamanisha na upande wako. Kitu cha kutulisha sisi, kukukoleza. Hicho ndicho tunachohitaji. Je, unaamini hilo? Kweli.

172 Mungu ana njia iliyoandaliwa. Je, uko ndani Yake usiku wa leo? Je, umepokea Roho Mtakatifu tangu ulipoamini? Sasa ninyi marafiki zangu wazuri wa Kibaptisti, na mnajua ya kwamba mimi nilikuwa mfuasi... Nilikuwa Mbaptisti, na mchungaji wangu hapa ni Mbaptisti. Lakini nataka kuwaambieni jambo fulani. Matendo 19 inasema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?” Sio *wakati* mlipoamini, bali “tangu” mlipoamini. Naam, bwana. Kama bado, ni kwa ajili yako usiku wa leo. Mungu anayo njia iliyoandaliwa.

173 Ndugu, dada, usijaribu kwenda njia yako mwenyewe. Usipitie kwenye majani ya mtini. Usiende ukielea kwenye gogo, kama walivyojaribu kufanya katika maangamizi yaliyotangulia

ile gharika. Usivae majani ya mtini, kama Adamu alivyofanya. Usijaribu kupitia njia ya Mfalme Nebukadreza, kulitesa Kanisa la Mungu. Usipitie njia hizi zote mbalimbali, taratibu hizi na njia hizi, ambazo tungeweza kutaja nyingi.

¹⁷⁴ Usiende kama Mafarisayo walivyofanya, mtu wa kidini sana, kasema, “Sasa angalia hapa, tuko mahali pa juu. Na ikiwa kuna chochote kinachoelekea, tutajua yote kukihusu.”

¹⁷⁵ Naye Mungu akaingia huko kisiri, na kumzaa Mtoto katika hori ya kulia ng’ombe Bethlehemu, akamshusha ulimwenguni; na kutoka duniani, adhabu ya kifo; wala hawakujua lolote kulihusu. Kweli! Njia ya Mungu iliyoandaliwa.

¹⁷⁶ Loo, wakati mmoja kulikuwa na mwanamke, alikuwa ametumia pesa zote alizokuwa nazo. Haleluya! Madaktari hawangeweza kumsaidia chochote. Na siku moja karibu azimie. Alikuwa ametokwa na damu kwa miaka mingi, mingi sana. Ndipo siku moja akasikia mngurumo ndani ya mashua. Alitazama nje, na hapo ilikuwa imekuja njia iliyowekwa na Mungu! Hiyo ni...?...Loo, jamani!

¹⁷⁷ Ninaweza kumwona akishuka kwa Wabaptisti wa tabaka la juu sana. “Siku za miujiza zimepita.” Alitambaa tu katikati ya miguu yao. Ilibidi wasonge.

¹⁷⁸ Ninamwona akija pale kwa Brigham Young na wake zake wote; alipita tu moja kwa moja. Alisema nini?

¹⁷⁹ Nawasikia wakisema, “Simama hapo! Unaenda wapi, yule tabibu hawezi kukusaidia chochote? Utaenda wapi basi? Nilikuona kule chini, ukiwa na kutokwa huko kwa damu.”

Akasema, “Ninapitia kwenye njia ya Mungu iliyoandaliwa.”

¹⁸⁰ “Iko wapi? Humaanishi yule mnafiki pale?”

“Hapo ndipo ilipo. Ninaipitia moja kwa moja.”

¹⁸¹ Akajipenyeza akapita, na kando kando, mpaka akamfikia jamaa huyu hapa. Na alikuwa wa—wa kanisa la namna *hii*, na *hii* na *ile*, nao wote wakajaribu kumsukuma nyuma. Lakini akafika kwa Yesu.

¹⁸² Baadhi yao wakasema, “Sasa ngoja kidogo, dada. Ikiwa unakula nyama, hutafaulu.” Alikuwa akipitia njia ya Mungu iliyoandaliwa.

¹⁸³ “Ikiwa hujashika nyoka, huwezi kufanya hivyo.” Alikwenda kwa njia ya Mungu iliyoandaliwa. Alitaka kufika kwa Yesu. Hiyo ni kweli.

¹⁸⁴ Ninamwazia Daudi wa kale. Haleluya! Naam, bwana. Aliposema ipo...Ambapo alizungumza kuhusu...Alisema, “Onjeni mwone Bwana ni mwema. Ina ladha ya asali mwambani.” Maelezo madogo ya kale niliyokuwa nikitumia, nikifikiria juu ya mkoba wa kale waliokuwa wakibeba ubavuni mwao *hapa*, kigunia kidogo walichoweka asali

ndani, wachungaji wa kale waliweka. Na wakati wagonjwa wangetoa... kondoo wote wangeshikwa na ugonjwa, wangetoa asali kidogo kutoka kwenye huo mkoba na kuimiminia juu ya jiwe la chokaa, na kumwita kondoo mgonjwa na kumwacha huo kondoo mgonjwa aende kulamba kwenye mwamba huo. Nao walipoanza kulamba asali kutoka mwambani, alikwenda na kulamba baadhi ya chokaa wakati akilamba asali. Nanyi mnajua kilichotokea? Hao kondoo wagonjwa wakapona.

¹⁸⁵ Sasa angalia hapa, ndugu. Nina mfuko mzima uliojaa Hiyo, usiku wa leo. Nami sitaiweka kwenye kanisa la Baptisti, kanisa la Methodist, kanisa la Presbiteri, ama kanisa la Kipentekoste. Ninaiweka juu ya Kristo Yesu, pale inapostahili, nanyi kondoo wagonjwa anzeni kulamba na mna hakika kupata kitu kutoka Kwake. Naam, bwana. Mlambe Yeye. Kama yule mzee, uzikwe, na...?... Mlambe Yeye; utaipata.

¹⁸⁶ Usizingatie kile ambacho kanisa lako linasema. Mzingatie Kristo. Mfuate Yeye, kwa maana, ndani Yake, Yeye ni Kanisa! Sawa, pitia njia ya Mungu iliyoandaliwa. Yeye kamwe hakusema Methodist ilikuwa njia ya Mungu iliyoandaliwa, wala Yeye hakusema Baptisti ilikuwa, ama kanisa lingine lolote. Alisema, "Mimi ndimi Njia, Kweli, na Uzima."

Unasema, "Vema, nitajuaje kuwa niko ndani Yake?"

¹⁸⁷ "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, kuwa washiriki wa Mwili huo." Wakorintho wa Kwanza 12, hiyo ni kweli, kutiishwa chini ya ninii ya Mungu...

¹⁸⁸ Kila kitu alichu nacho katika Ufalme Wake ni chetu. Anachukua tu kile Kitabu kikubwa kilichojaa hundi, na kutia sahihi Jina Lake hapo chini, anasema, "Haya basi, mwanangu. Chochote unachohitaji, nenda ukichukue." Amina.

¹⁸⁹ Usiogope kuijaza. Ijaze na uikabidhi, useme, "Asante, Bwana." Haleluya! Itakuja kutimia.

¹⁹⁰ "Chochote mtakacho," Marko 11:24, "mwombapo, aminini kuwa mtakipokea, kitakuwa chenu."

¹⁹¹ Tia cheki sahihi, useme, "Bwana, ninahitaji uponyaji." Ikwangu, useme, "Haya basi, Bwana, ninaomba katika Jina la Yesu uponyaji." Useme, "Asante, Bwana," na uendele mbele moja kwa moja, uamini kwa ajili ya uponyaji. Nayo inarudi moja kwa moja, kama hao kunguru wakishuka kumpelekea Eliya chakula hicho. Haya basi.

¹⁹² Useme, "Nahitaji wokovu kwa ajili ya nafsi yangu." Utafanya nini? Andika tu na kusema, "Kasema, 'Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo; nitawapa pumziko.' Hiyo ni kwa ajili yangu, Bwana." Jaza hiyo hundi. "Nahitaji wokovu. Nikabidhi mimi, Bwana."

"Hii hapa."

"Asante, Bwana." Ondoka nayo.

¹⁹³ Je, unahitaji Roho Mtakatifu? Naam, bwana. “Ngojeni katika mji wa Yerusalemu mpaka mtakapovikwa Uweza utokao Juu. Roho Mtakatifu akiisha kuja juu yenu, mtakuwa shahidi Wangu katika Yerusalemu, Uyahudi, na Samaria, na pande za mwisho za dunia.” Mnaamini Hilo? Ijaze hiyo hundi na uitume juu, imetiwa sahihi, uone kitakachotokea. Mungu ataitoa Hiyo. Njia ya Mungu iliyoandaliwa. Alikupa Kitabu cha hundi, kijaze. Mungu aliahidi Hilo. Je, unaamini hilo? Hakika. Mungu sikuzote ana njia iliyoandaliwa.

¹⁹⁴ Kulikuwa na maskini jamaa mmoja jina lake Yairo, siku moja. Loo, kwa namna fulani alikuwa amejiunganisha na kundi la wasioamini.

¹⁹⁵ Kama wahubiri wengi, wameunganishwa kwa njia ile ile siku hizi. Biblia ilisema “Usijifunge nira miongoni mwa wasioamini.” Vema. Muda si muda mnajua. . .

Unashangaa ni nani aliyesema hivyo? Unashangaa?

¹⁹⁶ Vema, Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Katika Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya, watashika nyoka, watakunywa vitu vya kufisha; wataweka mikonjo juu ya wagonjwa, watapata afya.” Ukihubiri Hilo, katika nusu ya makanisa, leo, wangekutoa nje ya mlango. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Sijui njia iliyowekwa na Mungu, lakini hivyo ndivyo alivyosema. Hivyo ndivyo Yesu alisema. Je, unaamini hilo? Naam, bwana.

¹⁹⁷ Na basi kama Yeye alisema hivyo, amina, ninaamini. Nafikiri ni Kweli, nami ninatembea katika njia Yake, yale Yeye alivyosema yafanywe. Naye analithibitisha kwa ishara, maajabu, yanayofuata. Hiyo ni kweli.

¹⁹⁸ Kwa hivyo fanya vivyo hivyo tu, ingia ndani moja kwa moja. Ni kwa kila. . . Atakaye na aingie. Njoo. Mungu amekuita, huna budi kuja, kwa hiyo ingia moja kwa moja ndani. Usingoje tena. Ichukue, usiku wa leo.

¹⁹⁹ Ninamwona maskini jamaa huyu; alijiunga mwenyewe. Alimpenda Yesu, lakini bado kidogo alikuwa tu. . . Hakutaka kupoteza heshima yake, mnajua, baraka. Kwa hiyo wanatoka; walitoka.

²⁰⁰ Kwa hiyo Bwana akasema, “Sasa mwangalie maskini jamaa huyo mdogo kule chini. Nilimchagua tangu awali kwa Uzima wa Milele, naye huyo hapo pamoja na kundi hilo la wasioamini. Kwa hivyo nitamrekebisha.” Alimwacha tu binti yake awe mgonjwa.

Akasema, “Vema, nitamwita Daktari Doe.”

²⁰¹ Daktari Doe akamtazama. Akasema, “Mapigo ya moyo yanapungua, Yairo. Hebu nikwambie tunachopaswa kufanya; afadhali tufanye *hivi, vile*.” Naye akampa dawa zote, na kadhalika. Aliendelea moja kwa moja, akifa.

202 Kisha akasema, “Si—si—si—sijui kama Mungu ana njia iliyoandaliwa?” Loo, jamani!

203 Mtu ambaye alikuwa amemkosoa sana, kuhusu uponyaji wa Kiungu! Au, aliyesikia habari Zake, akasema, “Naam. Naam. Uh-huh.”

“Yairo, hudhanii Yeye ni mnafiki?”

204 “La,” akasema Roho Mtakatifu, “Yeye si mnafiki. Unamwamini.”

205 “Loo, vema, naam. Loo, na—na—nadhani ndivyo alivyo.

206 Unaona, hivyo ndivyo baadhi ya wahubiri hawa wakwamia mpakani walivyo, hiyo ni kweli, wanaogopa tu. Loo, Mungu akuondolee mfupa wa shingo ya kuku akuwekee uti wa mgongo!

207 Ninapenda ushuhuda wa Buddy Robinson ulivyo. Alisema, “Bwana, nipe uti wa mgongo ukubwa wa gogo la msumeno. Weka kelele nyingi kwenye mwisho wa nafsi yangu. Na jalia nipigane na ibilisi mradi tu nimesalia na jino moja, kisha nimwume kwa ufizi mpaka nife.” Naupenda huo. Hiyo ni kweli. Akasema, “Nilikuwa na mbwa mzee. Alikufa, mkongwe. Alileta kuuni mpaka hakusaliwa na jino moja, basi yeye akawauma hao kuuni kwa ufizi wa meno, na kulia.” Napenda hilo. Kweli! Haleluya!

208 Unasema, “Ndugu Branham, karibu sikupata elimu nyingi. Mimi ni mdogo sana. Wahubiri watanikataa!”

209 Hebu turudi kwenye hiyo hadithi. “Sio ukubwa wa mbwa katika mapambano; ni ukubwa wa mapambano katika mbwa.” Ndivyo ilivyo leo! Simama hapo! Sikulinganishi na mbwa, lakini simama hapo.

210 Kama vile yule chifu mzee alivyosema siku moja, alipokuwa akijiandaa kuondoka. Kasema, “Unaendeleaje, chifu?”

211 Kasema, “Nataka kukwambia, ndugu.” Kasema, “Kunao mbwa wawili ndani yangu. Mmoja ni mweusi na mwingine ni mweupe. Yule mweusi anataka nitende mabaya, naye mweupe anataka nitende mema.” Kasema, “Daima wanapigana na kugombana.”

Nikasema, “Ni yupi hushinda, chifu?”

Kasema, “Inategemea ni yupi chifu anamlisha zaidi.”

212 Na hiyo ni kama kweli, pia. Naam, bwana. Vema, ndugu. Ninakwambia, kile ulimwengu unachohitaji usiku wa leo ni mtikiso mzuri wa kale.

213 Yairo akasema, “Sasa ngoja kidogo.” Binti akawa mgonjwa sana. Tumaini pekee lililokuwako, kumpata, lilikuwa ni kumwendea Yesu. Yeye. . . Wakaondoka kumwendea Yesu.

214 Akiwa njiani. . . Ninamwona akija huko juu. Na yule mwanamke ndiyo kwanza aponywe kutokwa na damu. Huyu hapa anaendelea, akasema, “Binti yangu amelala sasa. . . Sijali kasisi anasema nini, kile mtu yeyote mwingine anasema. Je,

utakuja, uweke mikono Yako juu yake? Ninaamini Wewe ni njia ya Mungu iliyoandaliwa kwa ajili ya uponyaji wake. Waweza kuja, uweke mikono Yako juu yake, apate afya?”

Kasema, “Nitakwenda.”

²¹⁵ Huyu hapa anaanza, akiendelea. Jambo la kwanza mwajua, huyu hapa mtu anakimbia kutoka nyumbani kwao, akisema, “Yairo, usimchoshe Bwana, kwa sababu, tayari amekufa.” Loo, loo, jamani! Ninaweza kuona maskini moyo wake ukiruka ndani yake, namna hiyo.

²¹⁶ Ninaweza kuona yale macho ya kupendeza, ya huruma ya Yesu yakimtaazama, kusema, “Je, sikusema, ‘Usiogope, nawe utauona utukufu wa Mungu?’” Yeye ndiye njia ya Mungu iliyoandaliwa.

²¹⁷ Kulikuwa na mzee mmoja jina lake Bartimayo kipofu, ameketi malangoni siku moja, akiomba sadaka. Kulikuwa na hali baridi ya hewa, yapata Oktoba. Akasikia kelele ikishuka barabarani. “Ni nini hiyo?”

“Mbona,” akasema, “hiyo ni—ni Yesu wa Nazareti.”

²¹⁸ Hakuwahi kutazama... Akavua joho lake. Yeye kamwe hakuliweka chini, na kulikunja hivyo, mnajua, angeweza kupata njia yake ya kuirudia kipofu. Akalitupa joho lake kando. Mungu alikuwa ameandaa njia, naye alikuwa akiifuata. Alikuwa amekimbia huku chini.

²¹⁹ Baadhi...?... kasema, “Kaa chini! Kaa chini! Hana wakati wa kujipumbaza nawe.”

²²⁰ Akapiga kelele kwa sauti kubwa zaidi, “Yesu, Mwana wa Daudi, unirehemu! Nirehemu!” Alikuwa akijipenyeza. “Nirehemu! Ninajua Wewe ni njia ya Mungu iliyoandaliwa kwa ajili ya macho yangu. Ee Bwana, nirehemu!” Hiyo ni kweli.

²²¹ Nilisoma historia ya kipofu Bartimayo, siku moja, hadithi ndogo. Walisema kwamba alikuwa kipofu kwa miaka mingi. Alikuwa na binti mdogo ambaye hakuwa amewahi kumwona. Usiku mmoja... Naye alikuwa akienda kule na kuketi mtaani. Alikuwa na mwana-kondoo mdogo. Wana-kondoo walikuwa wakiwaongoza vipofu kama mbwa wanavyofanya leo; mbwa huwaongoza vipofu. Walikuwa na mwana-kondoo aliyefunzwa kuwaongoza vipofu. Na kisha mmoja akasema, siku moja, kwamba...

²²² Alikuwa na njiwa wawili wadogo na wangepanya vitimbi vidogo, namna *hiyo*, kuvutia usikivu wa watalii, wakiingia Yerusalemu, au kuingia m—mjini, nao wangetia sarafu katika kikombe chake. Alikuwa kipofu.

²²³ Kwa hiyo usiku mmoja mke wake akaugua sana, kwa hiyo akamwendea Bwana. Naye akasema, “Bwana, sina chochote. Mimi ni maskini. Mimi ni kipofu. Sina cha kukupa Wewe. Lakini ninakuamini Wewe, Bwana. Na ikiwa utamhurumia tu

na kumwacha maskini mke wangu aishi, kesho nitakutolea njiwa wangu dhabihu.” Bwana akamponya mke wake usiku huo.

224 Kesho yake akarudi, kupitia kwa kuhani, akawatoa hao njiwa wawili dhabihu. Basi hakuwa na kitu ila yule mwana-kondoo.

225 Si muda mrefu baadaye, msichana wake mdogo akaugua. Madaktari wasingeweza kumfanyia lolote. Akasema, “Bwana, nimebakiza kitu kimoja tu,” na kusema, “hicho ni huyu mwana-kondoo. Lakini kama utamruhusu msichana wangu mdogo, ambaye sijawahi kumwona, kama tu utamruhusu apone, basi nitakutolea mwana-kondoo wangu dhabihu.” Basi Bwana akamponya msichana wake mdogo.

226 Siku chache baadaye, akaanza kupanda barabarani, yule mwana-kondoo akimwongoza. Naye Kayafa, kuhani mkuu, akaja, akasema, “Kipofu Bartimayo, unakwenda wapi?”

227 Akasema, “Ninaenda, Ee kuhani mkuu, hekaluni. Mwana-kondoo ananiongoza hekaluni; kumtoa mwana-kondoo dhabihu.”

“Loo,” akasema, “huwezi kufanya hivyo.”

Kasema, “Naam,” Bartimayo.

228 Akasema, “Hapa, nitakupa gharama ya mwana-kondoo. Nenda kanunue mmoja.”

229 Akasema, “Kamwe sikumwahidi Mungu mwana-kondoo *mwingine*. Nilimwahidi Mwana-kondoo *huyu*, mwana-kondoo huyu.”

230 Kasema, “Kipofu Bartimayo, huwezi kumchukua huyo mwana-kondoo. Mwana-kondoo huyo ndiye macho yako. Huwezi kuona bila mwana-kondoo huyo. Mwana-kondoo huyo anakuongoza. Huyo ndiye macho yako, kipofu Bartimayo. Huwezi kumtoa kafara mwana-kondoo huyo.”

231 Akasema, huyo mzee akatetemeka kidogo na kusema, “Ee kuhani mkuu, Mungu atatoa mwana-kondoo kwa ajili ya macho ya kipofu Bartimayo.”

232 Mungu aubariki moyo wake! Aliposikia hizo zikija; Mungu alikuwa ametoa mwana-kondoo. Huyu hapo.

233 Yeye ni Mwana-Kondoo wa Mungu aliyetolewa usiku wa leo. Yeye ndiye Mwana-Kondoo aliyetolewa kwa ajili ya macho yetu, macho yenu ya kiroho. Yeye ni Mwana-Kondoo aliyetolewa kwa ajili ya nafsi yako. Yeye ndiye Mwana-Kondoo aliyetolewa kwa ajili ya kukwepa kwako kuzimu. Yeye ni Mwana-Kondoo aliyetolewa kwa ajili ya utukufu wako Mbinguni.

234 Hivi hutampokea, tunapoomba, tunapoinamisha vichwa vyetu?

235 Ee Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, mwanzilishi wa Uzima wa milele, mpaji wa kila zawadi njema; tuma baraka

Zako juu ya watu hawa. Maskini matamshi haya madogo, yasiyotayarishwa, Bwana; lakini najua kuwa Wewe unayo njia iliyoandaliwa.

²³⁶ Ulisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Wakati wa maandalizi, wakati ambapo... Mahali pa kutayarishwa kwa ajili ya wale waliotaka kuepuka ghadhabu. Ninaomba, Mungu, kwamba sasa hivi, kwamba... Mwana-kondoo huyo wa Mungu aliyetolewa kwa ajili ya macho ya kipofu, au yule mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu, ambaye alikoma kutokwa damu, Mwana-Kondoo aliyetolewa kwa ajili ya Lazaro aliyekufa. Mungu, uturehemu.

²³⁷ Ninapofikiria juu yake, huyo ndiye Mwana-Kondoo yule yule aliyetolewa kwa ajili ya macho yangu mapofu, siku moja; Mayo Brothers waliponiambia, miaka mitatu iliyopita, sikuwa na tumaini la kuwa mzima tena. Mungu alitoa Mwana-Kondoo.

²³⁸ Wakati ulipomtuma Malaika Wako kule chini, kule kwenye Green’s Mill, na kusema, “Nenda, fanya hivi,” ningewezaje kufanya hivyo mbele ya ulimwengu mkubwa wa makafiri na wasiomini? Lakini Mungu alitoa Mwana-Kondoo.

²³⁹ Mungu, maskini kanisa langu hapa, Bwana, ninapolitazama! Nami nafikiri, maelfu ya maili kuvuka bahari, na nyanda zilizoganda na siwa barafu! Jinsi nilivyoketi pale, mara nyingi, katika chumba cha upweke, nikiomba. Nikiwazia wakati ambao wangekuja hapa na kunipa mkono. Unga wa mbao wa kale umetandazwa sakafuni, madirisha yakitikisika wakati upepo ulipovuma.

²⁴⁰ Ninawazia kumleta mke wangu mwenyewe kipenzi, na, kumlaza hapa chini ya msalaba, nikihubiri mazishi yake. Ninakumbuka kumwona mtoto wangu mchanga, Bwana, ambaye amelazwa juu ya mkono wake.

²⁴¹ Ninakumbuka maskini, maskini Billy Paul, ambaye Wewe ulimjaza Roho Mtakatifu saa chache zilizopita. Akishuka kwenye kaburi lake pale asubuhi hiyo, kuweka ua la Pasaka juu yake, naye akaanza kulia; nilimkumbatia huyo jamaa mdogo, na kusema, “Mungu ametoa Mwana-Kondoo, dhambi ya dhambi. Siku moja kaburi hili dogo litafunguka; mama atatoka, na pia dada mdogo. Mungu anaye Mwana-Kondoo aliyetolewa.”

²⁴² Baadhi ya siku hizi, Mungu, wakati mahubiri yangu ya mwisho yatakapohubiriwa; huenda akanilaza chumbani, nami ningehisi mapigo ya moyo yakipanda kwenye mkono wangu, wimbi baridi la kifo linaelea chumbani mwangu, dirisha likiwa wazi, mapazia yanavuma. Sukuma mashuaokozi basi, Bwana. Nitafanya safari yangu ya mwisho. Nitatandaza tu shuka. Kifuniko kitafungwa, nayo hiyo shuka itakuwa imenifunika.

²⁴³ Ninataka kushuka chini nipitie kwenye bonde la uvuli wa mauti. Nataka kuja Yordani, “Kueneka nje ya njia yangu!”

Na kupaza sauti, “Simile, Yordani! Navuka!” Bwana, sukuma mashuaokozi karibu nami basi. Unipokee, utanipokea, Bwana? Unipokee basi, sivyo, Bwana? Si mimi tu, bali kila mtu humu ndani, jalia apokelewe wakati huo, sivyo, Bwana? Lijalie. Tangu wakati huo, kungekuwa na wengi wetu tukivuka, na kurudi kwenye Paradiso na kisha kuishi milele.

²⁴⁴ Baba, kama kuna mwanamume huyo ama mwanamke hapa usiku wa leo asiyekujua Wewe, hajui thamani inahusu nini, hajapata kuzaliwa mara ya pili, kamwe hajapata njia ya Mungu iliyoandaliwa, jalia waipate sasa hivi, tunapoomba, kupitia Jina la Yesu Kristo.

²⁴⁵ Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, rafiki yangu mwenye dhambi. Mungu aubariki moyo wako. Wengi nje au ndani. Roho Mtakatifu yuko hapa. Je, umewahi kukubali njia ya Mungu ya kutoka, njia ya Mungu iliyoandaliwa kwa ajili yako? Hakuna unachoweza kufanya kustahili. Mungu ameiweka kwa ajili yako. Mbona usije, uipokee? Waweza kuja, usiku wa leo? Kama kuna rafiki mwenye dhambi hapa, inua mkono wako, useme, “Ndugu Branham, niombe. Nataka Mwanakondoo wa Mungu aliyetolewa maishani mwangu.”

²⁴⁶ Hatuna nafasi hapa ya wito wa madhabahuni kuyazunguka madhabahu. Hakuna nafasi, kwa hivyo ni kukuomba tu uinue mkono wako. Je, utafanya hivyo, mwenye dhambi? Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, bwana. Na Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, na wewe.

Huko nyuma, tena, kuna mtu yeyote huko nyuma?

²⁴⁷ Huku upande wangu wa kulia sasa? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mtu mwingine angeinua mkono wake, aseme, “Nikumbuke. Ee Mungu, nipe neema usiku wa leo, Uhai wa Mwana-Kondoo Wako.” Mungu akubariki, dada. Ninakuona, umeketi hapa.

²⁴⁸ Mtu aliye nje, njoo na uweke mikono yako kwenye skrini, na useme, “Ndugu Branham, nikumbuke. Nataka njia ya Mungu iliyoandaliwa.” 

52-0900 Njia Ya Mungu Iliyoandaliwa Kwa Ajili Yetu
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org